SALAMU FUPI ZA SHUKRANI ZA PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA BAADA YA KUAPISHWA MAJAJI SITA WA MAHAKAMA YA RUFANI TAREHE 23 MEI, 2023 IKULU CHAMWINO -DODOMA

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu;

Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi;

Wahe. Majaji wa Rufani;

Mhe. Mustapher Siyani, Jaji Kiongozi;

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu;

Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria, Wah. Mawaziri

Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi;

Wahe. Viongozi wote mliohudhuria.

SHUKRAN KWA MHE. SSH:

- Kutukaribisha Ikulu Chamwino, Jengo ulilolizindua tarehe 20/05/2023. Majaji 6 wa Rufani wamepewa heshima ya kupata nafasi ya kwanza ya uapisho katika jengo hili baada ya kuzinduliwa.
- Pongeza Mhe Rais, kwa kukamilisha ndoto ya ujenzi wa Ikulu Chamwino.

- Rais wa 28 wa Marekani, Thomas Woodrow Wilson, aliwahi kusema kuwa Kazi kubwa ya Viongozi ni kuota NDOTO kubwa, kuzitekeleza na kuzikamilisha. Nakupongeza kwa ndoto ya Jengo hili.

SHUKRAN KWA KUWATEUA NA KUWAAPISHA MAJAJI 6 WA RUFANI:

- Uwezeshaji Mkubwa, ilikuwa Historia ulipoteua Majaji hadi kufikia **25**. Umeongeza rekodi ya historia kwa kuongeza idadi hadi leo hii kufikia **31**.
- Ibara ya 118(1) imetaja idadi ya chini inayotakiwa ili nchi iwe na Mahakama ya Rufani—“Kutakuwa na Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Majaji wengine wasiopungua wanne (4), isipokuwa kwamba kikao maalum (FULL BENCH) kitakuwa na Majaji watano (5).

FAIDA—ONGEZEKO LA MAJOPO

- Mahakama ya Rufani hufanya kazi kupitia VIKAO vyenye majopo ya Majaji wa Rufani WATATU au WATANO, au SABA, kutegemea shauri husika.
- Majopo haya ndio hutoa huduma katika MASJALA KUU (DSM) na MASJALA NDOGO 17.
- Uteuzi wa Majaji 6 wa Rufani utaongeza idadi ya majopo ya watatu watatu kutoka Majopo saba (7) hadi Majopo tisa (9).

FAIDA—ZINGINE

- Kupunguza mzigo wa mashauri kwa kila jopo.
    - Hadi 30/04/2023, jumla ya mashauri ya rufani **5636** yalikuwa yamesajiliwa.Uwezo wa kila jopo la Majaji watatu watatu ni mashauri 33 kwa kikao kimoja. Kabla ya uteuzi wa Majaji wa Rufani 6, Majopo saba (7) yangegawana mashauri 5636 na wastani wa Mzigo kwa kila Jopo ilikuwa mashauri **805**. Baada ya Majopo kuongezeka hadi **9**, wastani wa mzigo kwa kila Jopo itashuka kutoka **805** hadi **626**.

FAIDA YA KUPUNGUZA MLUNDIKANO:

- Kuongeza majopo kutoka 7 hadi tisa, kutaongeza uwezo wa Mahakama ya Rufani kukamilisha na kupunguza mlundikano wa Mashauri ya Rufani.

FAIDA YA KUPUNGUZA GHARAMA KWA WANANCHI:

- Ongezeko la Majopo litaongeza idadi ya kutembelewa kwa Masjala Ndogo 17 za Mahakama ya Rufani na kupunguza gharama na umbali wa kufuata huduma Masjala Kuu DSM.

FAIDA YA KUONGEZA MASJALA NDOGO KULINGANA NA KUONGEZEKA KWA IDADI YA VITUO VYA MAHAKAMA KUU:

- Ujenzi wa miundombinu mpya za Mahakama itaongeza idadi za mashauri ya rufani yatakayofikishwa Mahakama ya Rufani kutoka vituo vya Mahakama Kuu.

MABORESHO YANAHITAJI KUFIKIRIA UPYA SHERIA NA TARATIBU TULIZOZOEA (RE-THINKING):

- Pamoja na jitihada zinazofanywa na Mhe. Rais za kuongeza idadi ya Majaji na matumizi makubwa ya TEHAMA Mahakamani ili kukabiliana na ongezeko kubwa la mashauri, Mahakama na Mfumo Mzima wa Utoaji Haki tunao wajibu wa kufikiria upya njia bora zaidi za kupunguza wingi wa mashauri mahakamani.
    - Lazima tufikirie upya hatua nyingi ambazo mashauri hupitia na kuziondoa zisizo na tija, na kuzifupisha ili kuharakisha usikilizwaji na ukamilishwaji wa Mashauri.
    - Hivi sasa kuna mashauri zaidi ya **200** ya Mabenki na Taasisi za Fedha; Mashauri ya ARDHI, Kuna mashauri **52** ya KODI; kuna mashauri ya Mirathi—ambayo imechelewa kwa sababu za taratibu za kimahakama zenye milolongo mingi na mirefu. Mashauri haya yamehodhi kiasi kikubwa cha rasilmali na kuchelewesha urahisi wa kufanya biashara na uwekezaji.
    - Nchi ya INDIA wamefanya *“RETHINKING”* na wamefupisha muda wa mashauri kuhusu Mabenki kubaki Mahakamani.
    - Wadau wote wa sheria Tanzania tunahitaji RETHINKING, na Mahakama peke yake haiwezi kukamilisha rethinking bila

wanaosimamia SERA na kutunga SHERIA kuona kuwa sheria zetu za utatuzi wa MIGOGORO inaleta misongamano na Ucheleweshwaji Mkubwa.
    - **“Nyumbu wa Serengeti-Masai Mara”**—Ni tofauti na sisi binadamu, na WANASHERIA sisi tunaweza kufanya RETHINKING.
    - Wah. Majaji Wapya wa Rufani lazima muwe mstari wa mbele kupendekeza Maboresho pale mnapoona kuwa TARATIBU zilizopo.

PONGEZI KWA MAJAJI WAPYA WA RUFANI KWA KUAMINIWA NA MHE. RAIS:

- Mtaishi Imani ya Mhe. Rais kwa niaba ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na KIAPO cha UAMINIFU KWA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA kwa kutambua:
    - Ibara ya 117 (3) inasema, *“Kazi ya Mahakama ya Rufani itakuwa ni kusikiliza na kutoa uamuzi juu ya kila rufaa inayowasilishwa Mahakama ya Rufani”*
    - Ina maana hiyo ndio jukumu letu kutekeleza kwa HAKI, bila HOFU, na bila KUCHELEWESHA.
    - Utamaduni wa Mahakama ya Rufani ni kuhakikisha unatoa Maamuzi yako katika Kikao ndani ya mud awa hicho kikao.
    - Wale wenzenu watakaoanza vikao—Musoma, Kigoma, Zanzibar na DSM kuanzia tatehe 28/5/2023 hadi 16/6/2023—watatoa maamuzi yao kabla hawajarudi DSM, na WATAPANDISHA hayo MAAMUZI TANZLII ili kila mtu atakayependa kusoma, atasoma hayo maamuzi.
    - Na kama JR ana uamuzi ambao utahitaji utafiti Zaidi, basi atoe uamuzi weake ndani ya SIKU 90 baada ya kusikiliza.
    - Ukichelewa Zaidi ya SIKU 90, warufani na wajibu rufani watakuwa na HAKI ya kupata maelezo!!!
    - Ukichelewa kupindukia, utaingia katika anga ya Ibara 120A (2) ya Katiba, *“Jaji wa Rufani anaweza kuondolewa katika madaraka ya kazi ya Jajhi wa Rufani kwa sababu ya **KUSHINDWA KUTEKELEZA KAZI** yake (ama kutokana na*

maradhi *au* ***sababu yoyote****) au kwa sababu ya TABIA MBAYA.”*

- Maradhi ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu ambaye hana makosa, lakini SABABU YOYOTE (kwa mfano uvivu) au TABIA MBAYA ni anga ambazo tusiiingie.

NAWAHAKIKISHIA UDUGU (COLLEGIALITY) YA HALI YA JUU KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI:

- Wiki mbili Baada ya UAPISHO ni muda wenu:
  - Kuonana na DEAN, na Wenyeviti wa Majopo kwa nasaha zao.
  - Mtaenda vituoni kukamilisha kuandika maamuzi yanayosubiriwa (Msiache Viporo vinavyoweza kuwaingiza katika dosari ya uchelweshwaji wa Hukumu)
  - Kuanzia tarehe 12 hadi 16 Mwezi Juni mtapata SEMINA ELEKEZI.
  - Baada ya SEMINA ELEKEZI mtapangiwa Mashauri na kushiriki katika MAJOPO.

MWISHO:

Nakushukuru Mheshmiwa Rais, kwa uwezeshaji huu.